JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA



CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0767492956**

**Makamu Mkuu wa Shule: 071466711**

**Matron/Patron: 0786727335**

**Shule ya Sekondari Pamba S.L.P 632.**

**Tarehe: 20/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**

**…………………………………………….**

**S.L.P ……………………………………..**

**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI PAMBA HALMASHAURI YA MWANZA JIJI MKOA WA MWANZA MWAKA 2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Tano** katika Shule hii mwaka wa masomo **2024/2025** na atasoma tahasusi ya ………….. Shule ya Sekondari **Pamba** ipo umbali wa Kilometa **moja** Mashariki mwa Mji wa **Mwanza**. Usafiri wa basi kutoka mjini Mwanza unapatikana katika kituo cha mabasi **Miti mirefu/Nata** Nauli ni Shilingi **200/=** kwa wanafunzi.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **01/07/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/07/2024.**



CamScanner

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

(a) Sare ya shule hii ni **Dark blue** yenye **Rinda box** mbele na nyuma kwa wasichana na **Suruali Nyeusi** kwa wavulana. Maelezo ya mshono yameambatanishwa.

(b) Rangi ya hijab (kijuba) ni **nyeupe**. Mshono umeambatishwa.

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni tracksuit rangi ya "**dark blue**" kwa wasichana na **dark blue** kwa wavulana. (Zitavaliwa muda wa michezo).

(d) Viatu vya shule ni **vyeusi** vya kufunga na kamba vyenye visigino **vifupi**

(e) Soksi jozi mbili **nyeupe ndefu mpaka magotini** kwa wasichana na kwa wavulana soksi nyeupe za kawaida.

(f) Mkanda wa kuvalia suruali ni **mweusi** wa ngozi

(g) Sweta **dark blue**

(h) Tai **dark blue (zinapatikana shuleni).**

(i) T-shirt (Zinapatikana shuleni)

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka **DOUBLE A;**
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
iv. Scientific Calculator;
v. Ufagio wa kudekia EGM, HGE;
vi. Mifagio (Hard brumes) CBG, PCM and PCM;
vii. Mifagio ya ndani miwili (soft brumes) HGL, HKL, HGK.
viii. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko; ix.Kwanja 1, jembe 1, reki 1

NB: Wanafunzi wote walete mifagio miwili ya chelewa.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a)Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **31102509852 School Fund Pamba Sec** katika **Benki** ya **NMB** (Tafadhali andika Jina la Mwanafunzi kwenye Pay in slip).

**Angalizo:** Jumla ya michango kwa wanafunzi wa kutwa ni Shilingi 50,000/=.



CamScanner

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na: i.Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii.Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule: ....[signature]....

Jina la Mkuu wa Shule: NAFTALI VITALIS MAGORI

Mhuri wa Mkuu wa Shule: MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI PAMBA
S.L.P. 632, MWANZA



CamScanner

NYONGEZA "B"

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI PAMBA**
**HATI YA KUKUBALI KUINGIA KIDATO CHA TANO**
**MWAKA 2024/25**

Mimi (Jina la Mwanafunzi)……………………………………nimepokea barua ya masharti ya kujiunga na shule ya Sekondari Pamba. Naahidi kutii amri zote halali zitakazotolewa na walimu na walezi wangu wengine shuleni. Nitafanya kazi zozote zitakazoiletea shule yangu na Taifa sifa nzuri, maendeleo na heshima.Nitafanya jitihada katika masomo yangu wakati wote. Naelewa kwamba wakati wote nitakapokuwa mwanafunzi nikifanya makosa yafuatayo nitafukuzwa shule.

1. Kuvuta bangi/ kunywa pombe au kutumia Madawa yoyote ya kulevya
2. Kuchelewa kufika shule/utoro
3. Kufanya mgomo, Kuchochea, Kuongoza au Kuvuruga amani na Usalama wa shule au wa watu.
4. Kujiunga na makundi ya wahuni
5. Kudharau Bendera ya Taifa
6. Kupatikana na mimba/kutoa mimba/kusababisha mimba (wavulana)
7. Uasherati na Ushoga
8. Wizi
9. Kupigana au kutishia kupigana ndani au nje ya shule na kutumia lugha chafu (matusi)
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
13. Kutovaa vazi rasmi la shule mf. Mlegezo, kutovaa Tai, Nembo na Sketi fupi.

**Saini ya mwanafunzi** ………………………………………………………………………… **Anuani** ……………………………………………………………………………………………

## SAINI NA UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi……………………………………… ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………… nakubaliana na masharti yote ya shule kama yalivyoainishwa hapo juu na ninaahidi kutoa ushirikiano kwa shule pale nitakapohitajika.

**Saini:** ……………………………………… **Tarehe:**………………………………………

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI PAMBA**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. **Jina lako:** ……………………………………………………
(Jina hili ni lazima libaki hivi hivi kwa miaka ijayo
Utakapokuwa shuleni)

Picha ya Mwanafunzi

2. **BABA:**
   a. Jina la Baba yako ni : ………………………
   b. Yu hai amefariki : ……………………………
   c. Kama amefariki lini : ………………………
   d. Anuani yake : ……………………………………
   e. Kazi na cheo chake: …………………………
   f. Dini ya Baba yako ni: ………………………
   g. Namba ya Simu: …………………………………

Picha ya Baba

3. **MAMA:**
   a. Jina la Mama yako …………………………
   b. Yu hai au amefariki …………………………
   c. Kama amefariki lini …………………………
   d. Anuani yake /cheo chake …………………
   e. Namba ya simu ………………………………

Picha ya Mama

4. Mlezi (i) Unaye mlezi ? Mlezi ni mtu asiye mzazi wako anayekutunza na kuhudumia kwa Chakula, Malazi n.k. NDIYO/HAPANA ……………………
(a)Jina la Mlezi huyu ni ……………………………………
(b)Uhusiano wako na Mlezi ni (Mjomba, Kaka, Rafiki, Shangazi (n.k)…..
(c)Anuani ya melzi wako ni …………………………
(d)Kazi ya mlezi wako ni ……………………………
(e)Namba yake ya Simu ………………………………

Picha ya Mlezi

5. (i) Jina la mtu atakayepelekewa ripoti zako za shule kama Baba/Mama au Mlezi wako ni ……………………………………………………
Anuani yake ni ……………………………………………………
Sahihi ………………………… Tarehe ……………………………
Namba ya Simu ……………………

SAHIHI YA MWANAFUNZI: ……………………………………
SAHIHI YA MZAZI/MLEZI: ……………………………………
JINA LA MZAZI/MLEZI: ……………………………………



CS CamScanner

NYONGEZA "D"

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANA**
**MNISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**
**PAMBA SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER IN RESPECT TO ALL FORM "V" ENTRANTS**

PUPIL'S FULL NAME ....................................................................................

AGE ........................................................................ SEX ......................

STOOL EXAMINATION ..............................................................................

BLOOD COUNT (RED AND WHITE) ..........................................................

URINALYSIS ..............................................................................................

SYMPHLIS TEST .........................................................................................

EYE TEST ...................................................................................................

CHEST .........................................................................................................

SPLEEN .......................................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION

(E.G Physical defects/impairment or chronic disease renquiring special treatment/attention)

..........................................................................................................................

I certify that I have examined the above pupil and recommend that he/she is fit/unfit to pursue Secondary Education.

Signed ..........................................................................................................

Designation ...................................................................................................

DATE: ............................... OFFICIAL STAMP ............................................

(Delete whichever is in applicable)

## TAARIFA YA MWANAFUNZI MAHALI ANAPOISHI

**JINA LA MWANZAFUNZI**………………………………………………………………

JINA LA MZAZI……………………………………………………………………

NO. YA SIMU YA MZAZI……………………………………………………………

**I. JINA LA MTENDAJI WA KATA**…………………………………………………

NAMBA YA SIMU ……………………

SAHIHI……………………………………

MUHURI…………………………………

**II. JINA LA MTENDAJI WA MTAA**………………………………………………

NAMBA YA SIMU ……………………

SAHIHI……………………………………

MUHURI…………………………………

**III. JINA LA MWENYEKITI WA MTAA**……………………………………………

NAMBA YA SIMU……………………


SAHIHI……………………………………

MUHURI…………………………………




CamScanner

UNIFORM (SURUALI):




- Rangi ya suruali ni NYEUSI
- Iwe na mfuko mmoja nyuma
- Shati la mikono mirefu Jeupe.
- Tai na sweta: dark blue
- Aweke alama ya “V” kwenye bega kuonesha kidato cha tano.

SKETI:



UNIFORM ( SKETI) RINDA BOX YA DARK BLUE


NB:

- Mfuko wa sketi uwe na zipu nyeusi au dark blue.
- Shati la mikono Mirefu la rangi nyeupe.
- Aweke bar (V) nyeusi begani kuonesha kidato cha Tano.
- Tai ya dark blue ifanane na rangi ya sketi.
- UREFU WA SKETI NI SENTIMITA 20 KUTOKA MAGOTINI KUSHUKA CHINI



CamScanner

UNIFORM (HIJAB)




**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0767-492956**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0714-667191**
- **Mwandamizi Taaluma: 0754-924639**
- **Mwandamizi Malezi: 0767-539225**



CamScanner